

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Barabara ya
Kilimatinde Cheyo,
S.L.P. 1020,
45112
TABORA,

Barua Pepe: rbctabora@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

TABORA 18 FEBRUARI, 2021

**ALIYEKUWA MENEJA WA TANESCO MKOA WA TABORA
KUFIKISHWA MAHAKAMANI**

TAKUKURU Mkoa wa Tabora kwa kushirikiana na ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali mnamo tarehe 18 Februari 2021 inatarajia kuwafikisha Mahakamani MOHAMED ABDALAH D'SOUZA- Aliyekuwa Meneja wa TANESCO Mkoa wa Tabora na MELKIAD JUAKALI MSIGWA – Mhandisi mwandamizi TANESCO kwa makosa saba ikiwemo Uhujumu Uchumi, kughushi, kutumia nyaraka yenye maelezo ya uongo, matumizi mabaya ya mamlaka na kuisababishia Serikali hasara.

Makosa hayo yalifanyika kati ya mwezi Desemba 2015 na Novemba 2018 ambapo MOHAMED ABDALAH D'SOUZA akiwa Meneja wa TANESCO Mkoa wa Tabora na MELKIAD JUAKALI MSIGWA akiwa Mhandisi Mwandamizi TANESCO Mkoa wa Tabora walitenda makosa ya kuendesha genge la uhalifu.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Tabora umabaini kwamba Melkiad Juakali Msigwa aligushi risiti kuonesha kuwa amenunua vifaa vilivyoorodheshwa kwenye risiti wakati wa ujenzi wa mradi wa kituo cha kupozea umeme kwenye mizani ya Puge Wilaya ya Nzega Mkoa wa Tabora.

Uchunguzi uliofanywa na TAKUKURU mkoa wa Tabora umethibitisha kwamba kati ya tarehe 10 Mei 2016 na tarehe 23 Juni 2016 MELKIAD JUAKALI MSIGWA akiwa Manispaa ya Tabora kama Mtumishi wa TANESCO Mkoa wa Tabora aligushi risiti yenye Namba 08645 na risiti namba 0078 kuonesha kuwa ni nyaraka halali kwa ajili ya kununua vifaa vya umeme vilivyoorodheshwa kwenye risiti aliyowasilisha huku akijua kuwa sio kweli.

Melkiad Juakali Msigwa kwa tarehe zisizojulikana mnamo mwaka 2016 akiwa Manispaa ya Tabora Mkoa wa Tabora kwenye ofisi za TANESCO aliwasilisha nyaraka zilizoghushiwa kutoka LESHEYA INVESTMENT COMPANY LIMITED na SOKO ELECRTICAL TRADERS kuonyesha kwamba vifaa vilivyoorodheshwa kwenye risiti namba 08645 na 0078 vilinunuliwa na SINOHYDRO CORPORATION LIMITED na kwamba nyaraka hizo ni halali huku akijua kuwa sio kweli.

Uchunguzi umethibitisha kwamba MOHAMED ABDALLAH D'SOUZA kwa nyakati tofauti kati ya mwezi Machi, 2016 na mwezi, Mei, 2018 akiwa meneja wa TANESCO Mkoa wa Tabora alitumia madaraka yake vibaya na kufanya maamuzi ya kujenga mradi wa kusambaza umeme kwenye mizani ya Puge kazi ambayo tayari iliidhinishwa na TANROAD ifanywe na M/S MAWENJENI ELECTRICAL CONTRACTOR na kujipatia manufaa isiyo halali ya kiasi cha Shs 20,492,600.72

Hivyo leo tarehe 18 Februari 2021 MOHAMED ABDALLAH D'SOUZA na MELKIAD JUAKALI MSIGWA watafikishwa Mahakamani kwa makosa saba ya kuendesha genge la uhalifu kinyume na Aya ya 4 (1) ya jedwali la kwanza ikisomwa pamoja na vifungu vya 57 (1) na 60 (2) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 Marejeo ya mwaka 2019, Kughushi kinyume

na kifungu cha 333,335(a) na 337 ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 Marejeo ya 2019, Kutumia nyaraka yenye maelezo ya uongo kinyume na kifungu cha 342 ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 Marejeo ya mwaka 2019, matumizi mabaya ya mamlaka kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 31, Aya ya 329 Marejeo ya mwaka 2019 ikisomwa pamoja na Sura ya 21 jedwali la kwanza na kifungu cha 57(1) na 60(2) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 Marejeo ya mwaka 2019

KATIKA HATUA NYINGINE TAKUKURU Mkoa wa Tabora leo tarehe 18 Februari 2021 itamfikisha Mahakamani NOEL HENRY MWAYA Mhasibu Chuo Cha Ufugaji Nyuki Tabora kwa kosa la ubadhirifu na ufujaji kinyume na kifungu cha 28(1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007.

Mtuhumiwa akiwa mwajiriwa wa Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora kama Mhasibu Msaidizi, alifanya ubadhilifu wa kiasi cha Sh. 3,664,000/=, fedha ambazo zilitakiwa kutumiwa kwa matumizi ya Chuo kwa ajili ya ununuzi wa mbao 160 za kutengenezea mizinga 60 ya Chuo iliyoko Wilaya ya Sikonge.

Ninawashukuru wananchi wa mkoa wa Tabora kwa ushirikiano mnaotoa kwa TAKUKURU. Tunawaomba muendeleo kutoa tarifa ya vitendo vya rushwa na kujitokeza kutoa kero kwenye mikutano ya TAKUKURU INAYOTEMBEA, katika maeneo yenu, vilevile wanachi tutumieni taarifa kupitia namba 113 au TAKUKURU APP nasi tunaahidi kuzifanyia kazi kwa weledi mkubwa.

Asante

Musa Chaulo

MKUU WA TAKUKURU MKOA